HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI

SHULE YA SEKONDARI
KOMSANGA
S.L.P 70,
HANDENI
15/12/2020

KUMB. Na KOMMS/PA/JI/20162017
JINA LA MWANAFUNZI.....

YAH: MAAGIZO NA MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA 2021 KOMSANGA SEKONDARI.

Nina furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Komsanga. Hivyo unatakiwa kuripoti shuleni hapa kuanza masomo ya muhula wa kwanza tarehe 11.1.2021 ufike saa1:00 asubuhi bila kukosa.

MAAGIZO MUHIMU KABLA YA KURIPOTI SHULENI

1. **SARE**

A)WAVULANA

- Suruali ya KIJANI iwe yenye rinda 2 na mifuko 3 na ambayo siyo MODO ukikiuka ushonaji hautasajiliwa kuanza masomo.
- Mashati mawili meupe mikono mifupi (yawetetroni)
- Viatu vyeusi vya kamba vya kisigino kifupi na soksi nyeusi

B.WASICHANA

- Mashati meupe mawili mikono mifupi (yawe tetroni)
- Hijabu rangi nyeupe (kwa imani ya dini tu)
- Viatu vyeusi vya kamba vya kisigino kifupi na soksi nyeupe
- Sketi kitambaa cha suti kizito rangi ya KIJANI Iwe na rinda box mbili na urefu wa sketi ivuke magoti na belt upana wa kawaida TAFADHALI Usikiuke ushonaji. Sketi fupi au kimini ni marufuku shuleni.

2. MAHITAJI MENGINE
   i. Fagio la chelewa moja kubwa
   ii. Daftari kubwa 11, mkebe 1 na kalamu za wino bluu au nyeusi na penseli.
   iii. Anatakiwa aripoti akiwa aje na
      a) Panga ,kwanja au jembe

ANGALIZO WAKATI WA USJILI NGUO NA VIFAA VINGINE VYA MASOMO VITAKAGULIWA

MAELEKEZO MENGINE

a) Hakikisha soma kwa makini sheria za shule na makosa na adhabu zake (sheria zimeambatanishwa)
b) Kwenda hospitali kwa ajili ya vipimo vya afya (fomu imeambatanishwa)
c) Fomu ya historian a ahadi kwa mwanafunzi na mzazi (fomu imeambatanishwa)

Tafadhali soma kwa makini maelezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

.....

JAPHARI .R. SHEKAONEKA

Kwa maelezo zaidi piga:

0716 592534/0622 258426

MKUU WA SHULE
KOMSANGA SEKONDARI
HANDENI

HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI
SHULE YA SEKONDARI KOMSANGA

TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi…… ……. Jinsia ……
2. Kidat…… mwaka ……
3. kabila……dini ……
4. Kuzaliwa tarehe ……Mkoa ……Wilaya …… Tarafa …… Kata …… kijiji ……
5. Kujiunga na shule hii mwaka …… Kidato ……
6. Namna ulivyojiunga na shule ya sekondari
   a) kwa kuchaguliwa kutoka shule ya msingi ……..
   b) Kwa uhamisho kutoka shule ya sekondari ……

7. Jina la Baba …… Kabila ……
   Dini ya Baba ……..
   Anaishi wapi? Kijiji /Mji …… Tarafa ……..
   Kazi ya Baba ……
   ……

8. Jina la mama ……kabila ……..
   Dini ya mama …….. YUHAI/AMEFARIKI
   Kazi ya mama ……..

9. Jina la mlezi(kama baba/mama huna)……..
   Mlezi anaishi wapi? Kijiji / mji
   Wilaya ya …… Mkoa……
10. Anuani ya mzazi/ mlezi ……
    .....

11. Makazi ya mwanafunzi KOMSANGA
    a) Unaishi wapi hapa KOMSANGA……
    b) Unaishi na nani anayekuangalia……
    c) Je unaishi mwenyewe kwa kupanga au kuishi kwenye nyumba ya ndugu bila mlezi yoyote? NDIO/HAPANA.
       Kama ndio eleza wazi ……
       ……
12. NATHIBITISHA TAARIFA NILIZOTOA HAPO JUU NI SAHIHI KABISA

    JINA……
    SAHIHI……TAREHE ……

HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI

SHULE YA SEKONDARI KOMSANGA

AHADI YA MWANAFUNZI.

1. Mimi .....nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote ambayo ni pamoja na sheria za shule na nimekubali kuingia kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Komsanga kuanzia tarehe ..... hadi nitakapomaliza masomo yangu.

2. Kwa hiyo naahidi kwamba :-
    a) Nitazitii sheria zote za shule na mambo yote muhimu yaliyotajwa .
    b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma ambavyo vitakua kinyume na sheria za serikali ya jamuhuri ya muungano wa tanzania.
    c) Nitatunza mali ya umma ambayo ni pamoja na majengo, samani (furniture) vitabu nk.

TAREHE ..... SAHIHI YA MWANAFUNZ.....

AHADI YA MZAZI MLEZI

Mimi .....mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo jii naahidi kwamba:-

1. Nitashirikiana na uongozi wa shule na walimu wote kwa ujumla katika kumuelimisha na kumlea motto wangu. Hii ni pamoja na kuhakikisha anazitii sheria zote za shule na kuyatimiza mambo yote muhimu.
2. Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu kufika shuleni kila siku kabla ya saa 1:15 asubuhi kwa masomo yake.

TAREHE .....SAHIHI YA MZAZI / MLEZI.....

SHULE YA SEKONDARI KOMSANGA

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu yenye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu

(c) Kutimiza kwa makini maandalizi ya jioni (Preparation)

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wa uanafunzi wako katika shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUSABABISHIA UKAFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati na Ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kuberi n.k.
5. Kupiga au kupigana
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau bendela ya Taifa
8. Kuoa au kuolewa
9. Kupata mimba, kutoa mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
10. Kugoma,kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.
11. Kukataa adhabu kwa makusudi.
12. Mwanafunzi kuwa na simu ya kiganjani wakati wa masomo hairuhusiwi.